# ATD DUNIA YA NNE TANZANIA
## *JARIDA*

Juni – Julai
Agosti 2015

Popote pale wanaume na wanawake wanapohukumiwa kuishi katika hali ya umaskini uliokithiri, haki za binadamu zimekiukwa. Kuja pamoja kuhakikisha kwamba hizi haki zinaheshimiwa ni jukumu letu makini.
- Joseph Wresinski (1917-1988) mwanzilishi wa ATD Dunia ya Nne -

## Tahariri

### Tambua, chukua hatua na lete mabadiliko



Rafiki Mpendwa

Tunafuraha kukutumia baadhi ya habari kutoka kwa wanachama wa ATD Dunia ya Nne. Tokea jarida letu la mwisho, tulipata fursa ya uzoefu katika matukio mbalimbali ambayo yalituwezesha kuimarisha uhusiano kati yetu.
Pamoja na mapambano yetu ya kila siku na watu wanaoishi katika umaskini, sasa tunashiriki katika changamoto mbili za muda mrefu. Katika uhalisia wake: nia ni kuelewa kwa undani maisha na mapambano ya watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri na kukusanya watu kutoka kila sehemu ya jamii na kuhakikisha lengo la mradi ni kwa wale wote wanaoishi katika umaskini uliokithiri..

Wanaharakati wa kujitolea wa ATD, na marafiki wa ATD wanaoishi katika umaskini na wasioishi katika umaskini wanahusika kusikiliza na kuelewa kile wanacho kieleza watu wanaoishi katika hali ya umaskini. Kisha wao watapendekeza watunga sera, kimataifa au kitaifa, wataalamu na wananchi katika kuzingatia uzoefu wa wale ambao hukabiliana na matatizo yaliokithiri.

Kufanikisha Elimu kwa Wote ni changamoto kubwa. Kama tulivyoelezea katika jarida lililopita, tunafanyakazi juu ya suala hili muhimu. Kamati inaundwa na wanachama wa ATD kutoka sehemu mbalimbali Tegeta, Tandale na Soko la Samaki la Dar es Salaam ambao wanafanya kazi hii. Rafiki yetu Selemani atazungumzia zaidi kuhusu hili kwenye ukurasa unaofuata.

Changamoto ya pili ni kutambua viashiria vipya vya umaskini katika mradi wa utafiti duniani kote. Kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Oxford pendekezo limeandaliwa kwa benki ya dunia kufadhili mradi huu mkubwa. Miradi hii mara nyingi mno huwatenga watu wenye uzoefu wa kuishi katika hali ya umaskini uliokithiri. Itakuwa nafasi kwa ajili yetu, nchini Tanzania, ili kukuza sera mpya na kutafuta njia mpya ya kuelewa hali ya kutengwa kwa kupitia uzoefu wa wale wanaoishi kwenye hali hiyo.

Tuko katika hatua ya awali. Kila mtu anaweza kushiriki katika suala hili, Karibu sana!!

Salehe Seif
Mwanaharakati kutoka katika timu

## Utafiti shirikishi juu ya vigezo vya umaskini

ATD Dunia ya Nne kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Oxford, ilianza mradi mpya ambao utashirikisha maarifa ya watu wengi, ufahamu juu ya umaskini na uelewa katika kutafuta viashiria vipya vya umaskini, katika nchi tano: Bangladesh, Bolivia, Canada, Tanzania na Uingereza.

Viashiria vya umaskini ni nyezo kwa ajili ya uelewa na kipimo cha umaskini. Mradi una lengo la kufafanua viashiria vilivyopo kwa kushirikiana na watu wenye uzoefu wa moja kwa moja wa umasikini, watendaji na wasomi, kwa kutumia mbinu inayojulikana kama kuunganisha maarifa, mizizi yake katika uelewa kwamba nyenzo muhimu ya maarifa ipo miongoni mwa watu wanaoishi katika umaskini na miongoni mwa wale ambao jukumu lao ni kukabiliana na umaskini.

**Viashiria vipya, uelewa mpya, sera mpya ....**

Inafahamika sana kwamba umaskini ni mkusanyiko wa mambo mbalimbali kama vile ukosefu wa rasilimali za kutosha ili kukidhi mahitaji ambayo yanayoendelea kuwapata watu walioathirika na umaskini. Pia inakubalika kwamba baadhi ya vipimo hivi si sahihi, kwamba vipimo fulani huenda hapo awali havikutambulika au vimekuwa chini ya sheria ya kukubaliwa na kwamba njia ambazo vipimo uingiliana kwa sura na uzoefu wa umaskini havikueleweka. Mapendekezo ya utafiti yamelenga juu ya masuala yote haya na kupitia maarifa ya watu ambao wanauzoefu wa umaskini moja kwa moja au wengine wanaofanyakazi pamoja na watu wanaoishi katika umaskini.



# Elimu kwa Wote

Utafiti wa elimu Kwa Wote sasa umefikia katika hatua ya Katikati ya mpango wake. Kama tulivyokuambia katika jarida la mwisho, utafiti huu shirikishi unalenga kuelewa hali gani ambayo itaruhusu watoto wanaoishi katika umaskini uliokithiri kuanza na kumaliza elimu yao ya shule ya msingi. Kamati ya wanachama ATD wanafanyakazi ya kuratibu. Salma na Hamisi, vijana wawili wa Kitanzania wanaharakati wa kujitolea wawezeshaji na wachangiaji wanatueleza kuhusu uzoefu wao..

**Je, wao hufanya nini?**

Moja ya majukumu yao ni kuwezesha Kamati ya utafiti, kundi linajumuisha watu wenye uzoefu na wasio na uzoefu wa umaskini. Kamati hii inafikiri, inaamua na kuchukua hatua kwa pamoja. Pia waliopo katika uwanja huu, *"Mimi niko pale kusaidia kufanya mahojiano "*, utafiti uliundwa ili kuruhusu watu wanaoishi katika umaskini kuwa watendaji wa mradi, Hamisi na Salma wanasaidia na ufanyakazi pamoja na kamati katika masuala mbalimbali ya mradi huo. Kwapamoja hutembelea watu wanaoishi katika umaskini kutambulisha mradi na kufanya mahojiano. Salma alisema, *"Mimi nina vutiwa na kamati kwa sababu tunafanya kazi kwa njia ya ushirikiano, tunasikilizana na kila mmoja na kusaidiana".*

**Kujifunza kwa vitendo**

*"Jambo la kwanza kubwa kwangu ni kwamba sijawahi kufanya kabla, kwa sababu inanifanya mimi najifunza mambo mengi. Mwanzo ilikuwa vigumu kwa sababu kwa kawaida utafiti unafanywa na wanataaluma, na vyuo vikuu, lakini kwa mimi, kupitia watu katika timu, kufanya kazi kwa pamoja ilinipa picha juu ya jinsi ya kufanya utafiti"*, anasema Hamisi. Kupitia mradi Salma anapata nguvu: *"Sasa ninajiamini kuzungumza na watu wengi"*.Hamisi anaelezea aligundua kuwa kupitia uzoefu wake wa kufanya kazi na familia zinazoishi katika mazingira magumu jinsi walivyo na wasiwasi na masuala ya elimu. Pia anatuambia kile cha kipekee kuhusu mradi huu ni, *"Hapo kabla tulikuwa na mradi wa upatikanaji kwa ajili ya Shule, tulitembelea familia na kusaidia watoto wao waweze kuhudhuria shule, lakini haikuwa hivyo kama utafiti huu ambapo huenda kwa kina katika kuelewa vikwazo vya familia hizo wanavyokabiliana katika kupeleka watoto wao shule, hapa tunakwenda zaidi"*. Salma na Hamisi watakuwa na furaha kushirikiana na wewe zaidi kuhusina na uzoefu wao, unakaribishwa kuuliza maswali. .

# AGENDA

**Tunakukaribisha katika ujio wa**
**Siku ya Kimataifa ya Kutokomeza Umaskini,**
**Oktoba 17, 2015 zingatia siku hii muhimu.**
**Unaweza kuungana nasi ili kujiandaa na siku hii.**

## Tambua, chukua hatua na lete mabadiliko



Selemani alikutana na ATD Dunia ya Nne mwaka 2003. Wakati huo anafanya kazi ya uvuvi na kuuza samaki na marafiki zake katika Soko la Samaki la Dar Es Salaam. Kwa sasa ni baba wa mtoto mmoja wa kiume, maisha yake ni mapambano ya muda mrefu lakini hatimaye aliweza kupata nafasi yake mwenyewe ya kuuzia samaki.
Selemani alihudhuria mafunzo ya elimu ya watu wazima mwaka 2009 yaliyotolewa na ATD kwa watu wanaofanya kazi katika soko la samaki na alifanikiwa kujifunza kusoma na kuandika kiswahili, ni kutokana na uzoefu wa maisha yake, yeye ni mtu mwenye kujihusisha sana na suala la mshikamano, upatikanaji wa haki kwa kila mtu na husaidia watu katika jamii yake inayomzunguka.

Alipopendekezwa kushiriki katika mradi wa utafiti wa Elimu Kwa Wote alisema, alihisi fahari kushiriki katika mradi huu na haraka alituambia: *"Tunahitaji kuzingatia elimu ya msingi kwa sababu kunachanga moto nyingi ambazo huzuia watu kuendelea na elimu yao, baadae, kama tutakuwa na rasilimali zaidi, tunaweza tukalenga ngazi ya sekondari"*. Kwa Selemani ilikuwa muhimu kujumuisha watu wa mtaani kwake anakoishi katika utafiti huu, pia watu anaojuana nao katika sehemu yake ya kazi na kufanya mahojiano nao.

*"Kabla sijakutana na ATD, sikuwa najiamini, leo naelewa vizuri njia ya kupambana na kila siku napiga hatua zaidi. Ndiyo maana naguswa pale ninapohisi kuna jambo linahusu watu hivyo sisiti kwa sababu inanikumbusha maisha yangu ya mwanzo na sitaki iwe hivyo kwa wengine".*

*"Sikujihusisha tu katika mikutano ya mara kwa mara, natumia muda mwingi kufikiri, kubadilishana mawazo na watu tofauti tofauti"*. Licha ya utofauti lakini watu huwa kitu kimoja. Ni fursa kubwa ya kupata mafunzo kama mtafiti. *"Zoezi hili limenipa uzoefu mzuri jinsi ya kufanya mahojiano"*, alisema Selemani baada ya hatua ya pili: kwenda kutembelea watu na kufanya mahojiano nao.

Kutoka kwake, *"Hatua zifuatazo zitakuwa na changamoto zaidi zinazowakabili familia zikiwa bado zina maswali kuhusu njia za kuwasaidia watoto na wazazi?"*. Kwa Selemani ni ushahidi: *"Upatikanaji wa elimu ni njia muhimu ya kuondokana na umaskini. Kama tutatafuta njia ya kutatua matatizo, familia zinaweza kuona elimu kama zawadi"*.

ATD Fourth World - P.O. Box 61786 - Dar es Salaam
Email : atd.tanzania@gmail.com
English website : www.atd-fourthworld.org/-Tanzania,549-.html
Tovuti ya Kiswahili : www.atd-fourthworld.org/-Kiswahili-.html